Ofisi ya Taifa ya Takwimu
S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz

*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/467

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 15 Agosti, 2012

# FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI JULAI, 2012

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEPUNGUA HADI ASILIMIA 15.7

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Julai, 2012 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Julai-2011 | Juni - 2012 | Julai-2012 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 115.75 | 140.63 | 139.86 | -0.5 | 20.8 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 104.48 | 116.07 | 123.32 | 6.2 | 18.0 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 106.98 | 122.14 | 122.97 | 0.7 | 15.0 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 118.29 | 130.96 | 133.10 | 1.6 | 12.5 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 112.68 | 122.19 | 122.53 | 0.3 | 8.7 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 101.83 | 105.06 | 105.56 | 0.5 | 3.7 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 110.18 | 115.25 | 115.40 | 0.1 | 4.7 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 98.15 | 96.54 | 96.58 | 0.0 | -1.6 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 100.62 | 112.07 | 112.59 | 0.5 | 11.9 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 105.79 | 110.75 | 110.75 | 0.0 | 4.7 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 108.76 | 126.83 | 126.25 | -0.5 | 16.1 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 103.26 | 114.68 | 114.45 | -0.2 | 10.8 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **112.51** | **130.06** | **130.19** | **0.1** | **15.7** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 114.98 | 139.11 | 138.37 | -0.5 | 20.3 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 128.50 | 146.05 | 149.46 | 2.3 | 16.3 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 109.57 | 119.34 | 120.51 | 1.0 | 10.0 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 106.73 | 115.32 | 116.16 | 0.7 | 8.8 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Julai, 2012 umeendelea kumepungua hadi asilimia 15.7 kutoka asilimia 17.4 kwa mwezi Juni, 2012. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi Julai, 2012 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Julai, 2012 imeendelea kupungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Juni, 2012. Hata hivyo, kwa ujumla Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 130.19 mwezi wa Julai, 2012 kutoka 112.51 mwezi wa Julai, 2011. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi kufikia asilimia 20.8 mwezi wa Julai, 2012 kutoka asilimia 23.5 kwa mwezi wa Juni, 2012.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 20.3 mwezi wa Julai, 2012 ikilinganishwa na asilimia 22.9 mwezi wa Juni, 2012. Kasi ya ongezeko la bei kwa bidhaa zisizo za vyakula imepungua kidogo hadi asilimia 10.0 kwa mwezi wa Julai, 2012 ikilinganishwa na asilimia 10.5 kwa mwezi wa Juni, 2012.

### Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Julai, 2012 umebaki kuwa asilimia 8.8 kama ilivyokuwa mwezi Juni, 2012. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei wa Nishati umepungua hadi asilimia 16.3 kwa mwezi wa Julai, 2012 kutoka asilimia 20.5 kwa mwezi wa Juni, 2012.

**Kielelezo Namba 1: Mwelekeo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Julai, 2011 Hadi Julai, 2012. (Septemba 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi kati ya mwezi Julai, 2011 hadi Julai, 2012, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyoonyeshwa na Fahirisi za bei. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kupanda kutoka asilimia 13.0 mwezi Julai, 2011 hadi kufikia asilimia 19.8 mwezi Desemba, 2011. Kuanzia mwezi Januari, 2012 mwenendo wa Mfumuko wa Bei ulianza kushuka kutoka asilimia 19.7 mwezi Januari 2012 hadi kufikia asilimia 15.7 mwezi Julai, 2012.

### MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 0.1

Mfumuko wa Bei wa mwezi Julai, 2012 umeongezeka kwa asilimia 0.1 kama ilivyokuwa kwa mwezi Juni, 2012. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 130.19 mwezi Julai, 2012 kutoka 130.06 mwezi Juni, 2012. Kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na; vinywaji vikali (Spirits) kwa asilimia 5.5, bia kwa asilimia 4.1, bidhaa za tumbaku kwa asilimia 14.3, mavazi kwa asilimia 0.6, viatu kwa asilimia 0.8, mkaa kwa asilimia 7.6, samani kwa asilimia 0.6, vifaa vya nyumbani aina ya nguo (household textiles) kwa asilimia 0.7, bidhaa za vioo kwa asilimia 1.7, dawa za kuulia wadudu kwa asilimia 2.4, huduma za afya asilimia 1.6 na; burudani na starehe

kwa asilimia 0.5. Japokuwa bei za bidhaa za chakula zimepungua kwa ujumla, baadhi ya bei za bidhaa za chakula zimeonyesha mwenendo wa kupanda kama bidhaa za kupikwa zitokanazo na unga wa ngano kwa asilimia 3.5, ulezi kwa asilimia 6.4, samaki waliokaangwa kwa asilimia 9.5, ndizi kwa asilimia 5.5, karoti kwa asilimia 11.2 na viazi kwa asilimia 3.2.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba, 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Julai, 2012

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imeendelea kupungua hadi Shilingi 76 na senti 81 kutoka mwezi Septemba, 2010 hadi Julai 2012

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Julai, 2011 hadi mwezi Julai, 2012. Kwa wastani, Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi na Fahirisi za nishati na mafuta zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonyesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**